

TFDA YAIBUKA MSHINDI KATIKA TAASISI ZENYE MIFUMO BORA YA UTENDAJI NA UONGOZI (BEST MANAGED INSTITUTION) WAKATI WA MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, 16-23 JUNI, 2011

1.0 Utangulizi

Kila mwaka ifikapo mwezi Juni, Tanzania huadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo huambatana na maonesho ya bidhaa na utoaji huduma kwa wananchi. Kwa mwaka huu wa 2011, maonesho wakati wa maadhimisho haya yalifanyika kuanzia tarehe 16-23 Juni, 2011 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam na yalikuwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka hamsini (50) ya Uhuru wa Tanganyika.

Madhumuni ya maadhimisho haya ni kuwawezesha wananchi kupata taarifa kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi mbalimbali za umma. Pia maadhimisho yanatumika kutoa elimu kwa umma juu ya masuala mbalimbali yanayohusu huduma za kijamii, kiuchumi na kisiasa.



Wananchi wakipata maelezo kuhusu kazi mbalimbali za Mamlaka kutoka kwa Bw J. J. Kyaruzi (mwenye miwani), wakati wa maonesho ya Wiki ya Utumishi, 16-23 Juni, 2011

Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ilikuwa ni *“Mkataba wa Kanuni za msingi wa Utumishi wa Umma Barani Afrika ni Chachu ya Kuimarisha Utoaji Huduma bora kwa Umma”* na maadhimisho ya mwaka huu yalikuwa ni mwanzo wa sherehe za maadhimisho ya miaka hamsini (50) ya Uhuru wa Tanganyika.

Pia maadhimisho ya mwaka huu yalikuwa ya Kimataifa kwa ngazi ya Afrika. Sherehe za maadhimisho zilienda sambamba na Mkutano wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa na Bara la Afrika kuadhimisha Siku ya Utumishi wa Umma Duniani, uliofanyika kuanzia tarehe 20-23 Juni, 2011 katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

2.0 Ushiriki wa TFDA kwenye Maonesho na Ushindani

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ilishiriki katika maadhimisho haya ya Wiki ya Utumishi umma kama sehemu ya kijiji cha Afya, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na taasisi zake.

Lengo kuu lilikuwa ni kutoa elimu na habari kwa umma kuhusu shughuli za udhibiti wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba nchini na taratibu za kupata huduma za TFDA. Aidha, ilikuwa ni fursa kwa Mamlaka kukutana moja kwa moja na wadau na wananchi na kujadiliana namna ya kuboresha utoaji huduma kwa lengo la kufikia matarajio yao bila kuathiri ubora na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Sambamba na kushiriki katika kutoa elimu na habari kwa umma, TFDA pia ilishiriki katika shindano la kutafuta Taasisi yenye Mifumo Bora ya Uongozi (Best Managed Institution) na Banda bora (Best pavilion) ambapo TFDA iliibuka Mshindi wa Kwanza (Best Managed Institution), katika kundi la Wakala za Serikali. Aidha, TFDA ilitangazwa kuwa Mshindi wa Jumla wa Taasisi zenye Mifumo Bora ya Uongozi (Overall Winner) kwenye kundi la Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na ilipatiwa vikombe na vyeti.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TFDA, Bw Hiiti B. Sillo akiwa ameshika moja kati ya vikombe viwili ambavyo TFDA ilikabidhiwa baada ya kuibuka mshindi wa kwanza kwa Taasisi yenye mifumo bora ya utendaji na uongozi (Best Managed Institution). Katikati ni Mgeni Rasmi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt Ali Mohamed Shein na kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bibi Hawa Ghasia.

Katika kundi la Wizara za Serikali, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliibuka Mshindi wa Kwanza katika shindano la banda bora (best pavilion). Kwa kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilishiriki kwa pamoja na taasisi zake, TFDA ni sehemu ya ushindi huu.

3.0 Hitimisho

Napenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ushindi huu mkubwa. Aidha, natoa shukrani kwa Wizara na Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa TFDA (MAB) kwa maelekezo na miongozo ambayo vimewezesha TFDA kupata mafanikio haya.

Shukrani za pekee pia ziende kwa Menejimenti ya TFDA na watumishi wote kwa ujumla kwa michango yao kwa kufanikisha ushindi huu, bila kusahau wadau wetu ambao wamekuwa wakishirikiana nasi kutoa michango, mapendekezo na maoni ya kuboresha utendaji kazi ndani ya Mamlaka.

Hiiti B. Sillo

MKURUGENZI MKUU